watuhumiwa mbalimbali wa vitendo vya rushwa wakati wa kura za maoni, uchaguzi wenyewe na baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2010. Sheria hii ina lengo la kudhibiti vitendo vya rushwa katika uchaguzi nchini kwa wagombea, wakala au wananchi kutojihusisha na vitendo hivyo.

Taasisi imeweza kuokoa kiasi cha shilingi bilioni 97.1 kwa kipindi cha 1995 hadi 2010. Kesi 770 zimefikishwa mahakamani baada ya Sheria Na.11 ya Kuzuia na Kupambana Rushwa ya mwaka 2007 kuanza kutumika, ambapo kesi 246 watuhumiwa wamepatikana na hatia na kuhukumiwa vifungo mbalimbali.

TAKUKURU imefanikiwa kufanya Utafiti na Udhibiti na kukusanya takwimu mbalimbali ili kubaini mianya ya rushwa na kuimarisha mifumo katika Wizara, Idara, Wakala wa Serikali na Sekta Binafsi. Ili jamii itambue umuhimu wa kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa, TAKUKURU imefanikiwa kuwafikia wananchi kwa njia za kisasa za uelimishaji. Njia zinazotumika ni redio, televisheni, semina, machapisho mbalimbali, gari la matangazo na luninga na ujumbe mfupi wa mapambano dhidi ya rushwa kupitia simu za mkononi.

Ili kujenga taifa adilifu, TAKUKURU imefanikiwa kushirikisha makundi ya jamii katika mapambano dhidi ya rushwa kama vile wasanii, wanafunzi kwa kuanzisha klabu za wapinga rushwa shuleni na viongozi wa dini. Tangu kampeni hii kuzinduliwa mwaka 2007 hadi Desemba 2010, jumla ya Klabu za Wapinga Rushwa 3,850 kati ya shule 3,852 zenye jumla ya wanachama 257,339 zimeanzishwa Tanzania Bara. Pia Februari 10, 2011 TAKUKURU imesaini makubaliano na Taasisi ya Elimu Tanzania ili kuhakikisha somo la rushwa linaingizwa katika mitaala ya elimu chini ili vijana wajengewe maadili na uzalendo mapema.

Aidha, TAKUKURU imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa Dhidi ya Rushwa na Mpango wa Utekelezaji Awamu ya Pili ambapo zimeanzishwa Kamati za Uadilifu katika Wizara, Idara, Wakala wa Serikali, Serikali za Mitaa na Sekta binafsi ili kusimamia uadilifu wa watumishi na kuzuia vitendo vya rushwa mahala pa kazi. Kutolewa mafunzo ya uadilifu kumewezesha kuanza kubadilisha mienendo ya watumishi.

Je, nini kifanyike ?

Pamoja na mafanikio hayo, TAKUKURU inatakiwa kufanya yafuatayo:-

- Kujenga na kuimarisha mifumo endelevu kwa ajili ya kufanikisha mapambano dhidi ya rushwa nchini.
- Kuimarisha na kuendeleza ushirikiano kati ya Serikali, Sekta Binafsi, asasi za kijamii na jamii katika mapambano dhidi ya rushwa.
- Kuendelea kuhimiza ushiriki wa viongozi katika ngazi mbalimbali za umma na kijamii katika mapambano dhidi ya rushwa.

Tuadhimishe miaka 50 ya Uhuru kwa kushiriki kuzuia na kupambana na vitendo vya rushwa.

Tanzania bila rushwa inawezekana, Chukua hatua'

Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, (TAKUKURU)
S.L.P 4865 Dar es salaam - Tanzania.
Simu: 022 2150043-6 | **Nukushi:** 022 2150047
Barua pepe: dgeneral@pccb.go.tz | **Wavuti:** www.pccb.go.tz

SIMU YA BURE 113

MIAKA 50 YA UHURU MAFANIKIO NA CHANGAMOTO ZA MAPAMBANO DHIDI YA RUSHWA

Utangulizi

Historia ya mapambano dhidi ya rushwa nchini imepitia katika vipindi mbalimbali. Kwa ufupi, mapambano haya yalianza kabla ya Uhuru mnamo mwaka 1930 chini ya utawala wa Kiingereza ambapo ulitumia Kanuni ya Adhabu ya India kuwaadhibu watumishi wa Serikali ya kikoloni waliopatikana na hatia ya kujihusisha na vitendo vya rushwa. Mnamo mwaka 1945 Sheria ya kwanza ya Kanuni ya Adhabu ya Tanganyika, Sura ya 16 ilianza kutumika kudhibiti vitendo vya hongo, kujipatia manufaa, limbikizo la mali na matumizi ya nyaraka zenye taarifa za uongo kwa lengo la kumdanganya mwajiri. Mwaka 1958 Sheria ya Kuzuia Rushwa, Sura ya 400 ilitungwa na kuanza kutumika.

Mapambano baada ya Uhuru

Desemba 9, 2011, Tanzania inaadhimisha miaka 50 ya Uhuru ikiwa na mafanikio na changamoto mbalimbali katika mapambano dhidi ya rushwa. Ili kukabiliana na changamoto hizo, Sheria ya Kuzuia Rushwa, Sura ya 400 imeendelea kufanyiwa marekebisho mbalimbali ambapo mwaka 1971 sheria hii ilibadilishwa kuwa Sheria ya Kuzuia Rushwa Na.16 ya mwaka 1971.

Januari 1975, Kikosi cha Kuzuia Rushwa kiliundwa kwa lengo la kuongoza mapambano dhidi ya rushwa nchini. Kikosi hiki kilikuwa chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani kabla ya kuhamishiwa Ofisi ya Waziri Mkuu na baadaye kuhamishiwa Ofisi ya Rais. Kikosi kilikuwa na jukumu la kuzuia rushwa, kupeleleza na kuendesha mashitaka dhidi ya watuhumiwa wa makosa ya rushwa nchini.

Mabadiliko ya Kikosi kuwa TAKURU

Kutokana na kukua kwa sekta binafsi miaka ya 1990 na kuanza kwa mfumo wa uchumi wa soko huria; mwaka 1991 jina la kikosi lilifutwa na kuanzishwa kwa Taasisi ya Kuzuia Rushwa (TAKURU) kwa tamko la Serikali Na.27 la mwaka 1991 ili kukifanya chombo hicho kifanye kazi zake kwa mbinu za kisayansi na uhuru zaidi. Wakati huo Taasisi ilikuwa na idara 3 ambazo ni Utawala na Utumishi, Sheria na Mashtaka na Mafunzo, Utafiti na Elimu kwa Umma.

Kuwepo kwa sheria za kupambana na rushwa kumetoa mwelekeo wa Serikali wa kupambana na rushwa nchini. Januari 17, 1996, Rais Mstaafu wa awamu ya tatu, Mhe. Benjamin William Mkapa aliteua Tume ya Warioba. Tume hii iliundwa na watu tisa (9) kuchunguza kero ya rushwa katika taasisi za Serikali ikiongozwa na Waziri Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Sinde Warioba. Kutokana na mapendekezo ya tume hiyo, sheria mbalimbali zimeboreshwa na mapambano dhidi ya rushwa yameshirikisha kila mmoja kwa nafasi yake.

Je, TAKUKURU inatokana na nini?

Kutokana na maendeleo ya sayansi, teknolojia na utandawazi, mwaka 2007, Sheria ya Kuzuia Rushwa Na.16/1971 ilifutwa na Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na.11/2007 ilianza kutumika rasmi Julai 01, 2007. Kutokana na Sheria hii, jina la Taasisi ya Kuzuia Rushwa lilibadilishwa na kuwa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa- TAKUKURU ambayo imepewa mamlaka ya kuchunguza makosa (24) ya rushwa kutoka makosa manne (4) yaliyokuwa yanasimamiwa na Sheria ya Kuzuia Rushwa Na.16/1971. Kwa sasa TAKUKURU ina Idara nne (4) ambazo ni Utawala na Rasilimali Watu, Uchunguzi, Utafiti, Udhibiti na Takwimu na Idara ya Elimu kwa Umma. Pamoja na Idara hizo, kipo kitengo cha Mipango, Ufuatiliaji na Tathmini kinachoongozwa na Mkurugenzi.

Ni namna gani TAKUKURU inafikia jamii?

Ili kufikisha huduma za TAKUKURU karibu na wananchi, Taasisi imeendelea kufungua ofisi mpaka wilayani. Awali Taasisi ilikuwa na ofisi katika Kanda tano (5) tu ambazo ni Arusha, Dar es Salaam, Mbeya, Dodoma, Mwanza na Tabora. Baadaye mwaka 1999 Taasisi ilifungua ofisi zake katika mikoa yote ya Tanzania Bara. Mwaka 2006 Taasisi ilianza kufungua ofisi katika ngazi ya wilaya ambapo sasa kuna ofisi 23 za mikoa na 90 za wilaya na vituo maalum 7.

Je, ni mafanikio gani yamepatikana?

Mapambano dhidi ya rushwa nchini yamekuwa na mafanikio kadha wa kadha. Ikumbukwe kuwa vitendo vya rushwa vinabadilika kulingana na wakati. Baadhi ya mafanikio ni kutanuka kwa ofisi hadi wilayani na kuboresha huduma kwa wananchi, kutungwa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya mwaka 2007 iliyoongeza wigo wa kushughulikia makosa ya rushwa kutoka manne hadi 24, kutoa ulinzi kwa watoa taarifa, wataalam na mashahidi wa uchunguzi wa vitendo vya rushwa.

Tanzania imeridhia na kusaini mikataba mbalimbali ya kimataifa ya mapambano dhidi ya rushwa ambayo ni Mkataba wa Umoja wa Mataifa Dhidi ya Rushwa wa mwaka 2003 na Mkataba wa Umoja wa Afrika ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ya mwaka 2003. Mafanikio mengine ni kuridhiwa Itifaki ya Nchi za Kusini mwa Afrika ya Mapambano Dhidi ya Rushwa ya mwaka 2001 na TAKUKURU kuiwakilisha Serikali katika Jumuiya ya Afrika Mashariki katika eneo la utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa kupitia Shirikisho la Mamlaka za Kuzuia na Kupambana na Rushwa za Afrika Mashariki (East African Association of Anti-Corruption Authorities-EAAACA). Hii ni hatua muhimu kwa kuwa vitendo vya rushwa na athari zake vinavuka mipaka ya nchi hivyo kuhitaji ushirikiano na nchi nyingine ili kuvidhibiti.

Mwaka 2010 Serikali ilipata msukumo mpya katika mapambano dhidi ya rushwa baada ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Jakaya M. Kikwete kusaini muswada wa Sheria ya Gharama za Uchaguzi na kuwa Sheria Na.6 ya mwaka 2010. Katika kutekeleza Sheria hiyo jumla ya kesi 10 zilifikishwa Mahakamani zikiwahusu